



TAARIFA KWA UMMA

Dar es Salaam, 06 Februari, 2025

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inawatangazia Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Watanzania fursa ya kutangaza na kuuza bidhaa za Tanzania katika soko la Kimataifa kwa njia ya Mtandao wa **e-Trade Desk**. Ili kuweza kunufaika na fursa hiyo, Kampuni inatafanyiwa uhakiki na kupewa namba maalum ya utambuzi ya kuingilia kwenye mfumo (*identification number*).

Hivyo, tunaalika kampuni mbalimbali za Tanzania zenye nia ya kuuza bidhaa Kimatiafa kuwasilisha taarifa zao za bidhaa zinazokidhi ubora wa kimataifa (content & package) pamoja na viwango vinavyokubalika kwa kujaza fomu maalum kupitia kiunganishi hiki;

<https://edodoso.gov.go.tz/index.php?r=survey/index&sid=615315&lang=en>

Aidha, ili kujua taratibu za kuuza nje ya nchi na kuingiza bidhaa nchini tembelea tovuti ya <https://trade.tanzania.go.tz>

Imetolewa na

Kitengo cha Uhusiano kwa Umma na Masoko
Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania